NDOA ZA UTOTONI

Herieth Makwetta, Mwananchi hmakweta@mwananchi.co.tz



Sheria ya ndoa bado changamoto

Binti niliyemfahamu miaka mitatu iliyopita akiwa darasa la saba, Antonia Sanga (si jina halisi) nimeshangazwa nilipomuona akiwa amebeba mtoto mgongoni lakini wakati huohuo akiwa na ujauzito.

Antonia mwenye miaka 16, aliolewa baada ya kuhitimu darasa la saba. Kwa sasa ana mtoto wa mwaka mmoja na miezi minane lakini ana ujauzito wa miezi mitano.

Huyu ni miongoni mwa wasichana wadogo mkoani Njombe, ambao wameolewa katika umri mdogo baada ya kushindwa kuchaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari.

Antonia ni miongoni mwa maelfu ya wasichana nchini wanakosa msaada wa kisheria kwa kuwa hawakuendelea na masomo, hivyo hupewa mimba za mapema na kuozwa ndoa za utotoni huku kukiwa hakuna sheria inayowatetea.

Asasi isiyo ya kiserikali ya Msichana Initiative mwaka 2016 ilishinda kesi baada ya kuishtaki Serikali kuhusu upungufu uliopo katika Sheria ya Ndoa za Utotoni ya mwaka 1971.

Hata hivyo, Serikali ilikata rufaa, lakini Oktoba 2019 Mahakama ya Rufaa ilitoa hukumu ikikubaliana na hukumu ya Mahakama Kuu ya mwaka 2016 kuhusu shauri hilo lililokosoa ndoa chini ya miaka 18.

Tangu hapo Serikali ilipewa mwaka mmoja kubadili sheria hiyo mpaka kufikia Oktoba 2020 iwe imetekeleza kwa kuwa Mahakama ilisema vifungu vya sheria vinavyoruhusu mtoto kuolewa ni batili inabidi vibadilishwe.

Mtandao wa kutokomeza ndoa za utotoni Tanzania (TECMN)unaounganisha mashirika zaidi ya 60 yanayofanya kazi katika kusaidia watoto kutokomeza ndoa za utotoni tangu mwaka 2012 na kuzifanyia kazi changamoto kwa pamoja, unasema shauri hilo halijafanyiwa kazi.

Mratibu wa mtandao huo, Euphomia Edward anasema kama wadau waliona kuna haja ya kuunganisha nguvu, rasilimali na uzoefu katika kukabiliana na ndoa za utotoni kuanzia mwaka 2012 wakafanya kazi kwa pamoja na kufanya uchechefuzi katika ngazi ya taifa hadi jamii.

Euphomia anasema pamoja na Msichana Initiative kuishtaki Serikali kuhusu Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, licha yavisababishi vingi vya ndoa za utotoni sheria hiyo ilikuwa mojawapo ya vyanzo vya ndoa za utotoni.

"Tuliona watoto wakiolewa miaka 14 mpaka 15,kwa hiyo na sisi tunatambua sheria na sera katika mkumlinda mtoto, ndiyo maana tangu sheria imeanza tumekuwa mstari wa mbele katika kupinga na kudai mabadiliko ya sheria ili mtoto abaki kuwa salama," anasema.

Euphomia anazitaja sababu zingine kuwa ni pamoja na umaskini, hivyo wengi wanawaoza mapema kupata mahari na kupunguza mzigo katika familia, lakini anataja visababishi vingine kuwa ni mila na desturi ikiwamo ukeketaji unaochochea binti kupata mimba na ndoa za mapema.

Anasema suala la usawa wa kijinsia bado ni changamoto, jamii inaona mtoto wa kike ameumbwa kuwa mke na sio daktari, mwalimu au mwanasheria.

"Kuna ile wazazi wanaona binti akipata mimba itakuwa aibu kwa familia anaamua kumuoza mapema bila kujali, umri, afya yake bado. Takwimu za mwaka 2016 zinaonyesha asilimia 36 ya wasichana wenye miaka 20 na 24 waliolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18.

"Mkoa wa Shinyanga unaongoza ndoa za utotoni kwa asilimia 59 waliolewa kabla ya kufikisha miaka 18, tabora 58, Mara 55, Dodoma 51 kwa hiyo tunaona bado chnagamoto ni kubwa. Kipindi cha katikati utafiti haujafanyika lakini tunaamini kipindi cha corona pia kuna ndoa za utotoni zilizaliwa," anasema Euphomia.

NUKUU

"Ndoa za utotoni haziwezi kumalizwa na mtu mmoja au na shirika moja, inahitaji maoni na ushiriki utakaojumuisha watu wengi kupitia jicho la kiafya, kiustawi na kiuchumi kila mtu aangalie kuona jukumu lake na wajibu wake kuanzia ngazi ya familia, jamii na Serikali kwa ujumla.

Jamii bado ina mkanganyiko na kutotekelezwa kwa hukumu kunatengeneza mwanya kwamba ndoa lazima ziendelee,

Wabunge wapya kuhakikishe wanaisimamia Serikali kutekeleza majukumu kwa kuwa wana wajibu wa kikatiba kuitaka Serikali kupeleka muswada bungeni kupitia mwanasheria mkuu wa Serikali, wizara ya katiba, wizara ya afya maendeleo ya jamii."

Gyumi

Hata hivyo, anasema kama wadau wameendelea kuongeza nguvu katika kupambana na visababishi vya ndoa za utotoni ikiwemo suala la sheria.

"Tumefanya uchechefuzi ngazi ya kitaifa tumekutana na wabunge mara kadhaa, mwanasheria mkuu wa Serikali, Spika wa Bunge la Tanzania na naibu spika kujadiliana nao hili suala lakini bado hatujafanikiwa," anasema

Euphomia.

Pia, anasema TECMN inashangazwa na ukimya wa Serikali inayotakiwa kufanya mabadiliko ya sheria ya ndoa ya mwaka 1971 ambayo wasichana wanaendelea kuolewa,

Anasema sheria ni sehemu moja lakini bado wadau hao wamejipanga kuendelea kuwekeza nguvu katika jamii ipate uelewa juu ya ndoa za utotoni, madhara, sababu na waweze kuwa mstari wambele kupinga na mabadiliko ya sheria yanapofanyika waweze kuelewa.

Pia, anasema tayari Mahakama imeshaweka wazi kuwa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ni batili na inamkandamiza mtoto wa kike, hivyo Serikali ambayo ndiyo mhusika mkuu au mwanasheria ni wakati wao sasa kubadili sheria hiyo.

"Mabadiliko haya yafanyike mapema kwa kuwa ni sheria iliyopo sasa inamlinda mtoto aliyepo shuleni pekee lakini kwa yule aliyepo nyumbani sheria imemtenga, yakifanyika mabadiliko ya pamoja yatawalinda wote kwa wakati mmoja.

"Kuwe na mazingira wezeshi ya wale ambao wameshindwa kuendelea na masomo, wapelekwe hata ufundi angalau muda usogee, lakini pia viongozi wa kidini na wa kimila pia wakague umri wa wale wanaowafungisha ndoa kuanzia kwenye vyeti vya kuzaliwa au vya kiraia ili kuweza kuwabaini wasichana wadogo wanaoingia kwenye ndoa za mapema," anasema Euphomia.

Mkurugenzi wa Agape, John Myola anaelezea madhara ya ndoa za utotoni katika jamii.

"Tamaduni nyingi za Kitanzania, wasichana wanadhaniwa kuwa tayari kuolewa wanapobalehe na ndoa inaonekana kama njia ya kuwalinda dhidi ya ngono na mimba za kabla ya ndoa," anasema Myola.

Anataja madhara ya ndoa za utotoni kuwa huweza kupelekea athari za kiafya kwa mabinti kwa kuwa wengi hupata mimba wakiwa bado na umri mdogo huku miili yao ikiwa haijapata uwezo wa kubeba mimba na kujifungua salama. Hii huweza kuhatarisha maisha ya mama na hata kichanga chake.

Anasema kwa watoto wasio na elimu au ujuzi wa kitaalamu wa kiuchumi wana uwezekano mdogo sana wa kuongeza kipato katika familia na huendeleza mzunguko wa umaskini utakaoathiri maendeleo ya watoto, familia na Taifa kwa ujumla.

"Ndoa za utotoni ni suala linaloathiri haki za watoto zaidi na kwamba haki hizi zinapuuzwa huku matokeo yanayotokana na vitendo hivi ya kizidi kuumiza idadi kubwa ya mabinti, nyingi ni za kulazimishwa na husababisha idadi yao kubwa kukatishwa masomo ili wakaolewe huku mabinti hawa wakinyimwa nafasi ya kuzungumza chochote katika uendeshaji wa maisha yao wenyewe," anasema.

Pamoja na hayo Myola anasema husababisha ongezeko kubwa la watoto waishio katika mazingira hatarishi, umaskini katika familia, kaya, jamii na Taifa kwa ujumla.

Mkurugenzi wa Shirika la Msichana Initiative ambaye ndiye aliyeishtaki Serikali kuhusu sheria batili ya ndoa za utotoni ya mwaka 1971, Rebeca Gyumi anasema walishinda kesi mwaka 2016 Serikali ilikata rufaa ambapo pia mahakama ilisema kwamba vile vifungu vya sheria vinavyoruhusu mtoto kuolewani batili inabidi vibadilishwe.

Hata hivyo alisema baada ya shauri hilo, Serikali ilipewa muda wa mwaka mmoja kuwa ibadilishe sheria hiyo mpaka Oktoba 2020.

"Ilibidi kupitia ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Bunge wawe tayari walishaanza hatua za kushughulikia mabadiliko hayo lakini hakuna kilichofanyika. Kisheria inapotokea hukumu inapewa muda kuwa imetekelezwa na muda unapopita vile vifungu vinakuwa vimefutika," anasema Gyumi.

Anasema wameendelea kushinikiza Serikali kupitia Bunge iendelee na mchakato kupitia wizara zinazohusika kama Wizara ya Sheria na Katiba.

Gyumi anasema maeneo ya Tarime, Mtwara na maeneo ya Nyanda za Juu Kusini matukio ya ndoa za utotoni hayawezi kuisha ikiwa sheria hiyo haitatekelezwa.